# Mwongozo kwa aliyekabiliwa na ubaguzi

Njia za kusuluhisha matukio ya ubaguzi

# Ufafanuzi mfupi wa ubaguzi

Ubaguzi kama dhana humaanisha utathmini wa kundi la binadamu linalodhaniwa kwa mfano kwa msingi wa asili, rangi ya ngozi, uraia, utamaduni, lugha mama au dini kama duni kuliko makundi mengine ya binadamu. Mara nyingi ubaguzi unaendana na dhana, kwamba kundi la mtu mwenyewe ni bora kuliko makundi ya wengine.

**Marejeo:**
Msalaba Mwekundu: Ubaguzi ni nini?
Yhdenvertaisuus.fi: Misamiati ya kupinga ubaguzi.

**Msaada na uungaji mkono kwa utambuzi wa ubaguzi:**

Anwani ya mtandao:
Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi: Misingi ya ubaguzi.

**Maelezo zaidi juu ya aina tofauti za ubaguzi:**

Anwani ya mtandao:
Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi: Ubaguzi.

**Walioshiriki katika utengenezaji wa mwongozo huu:**
Rovalan Setlementti ry (Chuo cha Rovala, Tamaduni mbalimbali MoniNet na Ofisi ya Usuluhishi ya Rovaniemi, Ranua na Posio, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai)
SPR Jimbo la Lappi
Mister's ry Kilabu cha Wanaume cha Utamaduni Mbalimbali
Rovalan Nuoret ry – Nyumba ya Wavulana
Mji wa Rovaniemi – Mradi wa International wa Rovaniemi (ESR+)
MIELI Rovaniemen seudun mielenterveys ry – Rovaniemen Neuvokas
M;ji wa Kemi – Huduma za Wahamiaji
MLL Jimbo la Lappi
Idara ya Polisi ya Lappi – Harakati za kuepusha



# Ubaguzi unaweza kutokea wapi?

Katika matukio ya shughuli na huduma

Kwenye maeneo ya umma

Kwenye mitandao ya kijamii, katika anga za burudani na michezo

Katika mambo yahusikayo na ufanyaji wa maamuzi ya kisiasa na mazungumzo ya umma

Kwenye vyuo vya elimu

Kwenye sehemu za kazi

Katika michezo ya kuburudisha na shughuli za muda huru

# Katika matukio ya shughuli na huduma



1



**Eleza kuhusu yale ambayo umepitia.**


Mtu akikutendea visivyofaa, mwambie anakosea namna gani.

2



**Omba mtu aache.**


## 3



**Ubaki na utulivu mwenyewe.**

Hisia zinaweza kupanda, lakini utulivu utakusaidia kuchukua hatua ya njia ya kueleweka na kwa kuleta matokeo.

## 4



**Toa taarifa kwa msimamizi.**

Kama tabia zisizofaa zinaendelea, uombe upate kuongea pamoja na msimamizi. Umweleze msimamizi yale yaliyotokea.

## 5

**Kama suala linashindikana kusuluhishwa, unaweza kuwasiliana na:**



- Baraza la Usawa wa Kijinsia na Kupinga Ubaguzi
- Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi
- Mchunguzi Maalum wa Kuwawakilisha Wagonjwa
- Mchunguzi Maalum wa Masuala ya Huduma za Jamii
- Senta ya Mikopo na Maendeleo ya Makazi (ARA)
- Huduma za Ushauri wa Bima na Fedha
- Pia unaweza kuomba ufafanuzi kutoka kwa mwajiri mwenye wafanyakazi ambao wamekutendea visivyofaa.


## 6

poliisi.fi/tee-rikosilmoitus

**Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**


Suala la jinai linaweza kutolewa ripoti ya uhalifu kwa Polisi. Panapohitajika, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai zinaweza kusaidia kuendeleza suala.

# Maeneo ya umma



**Rejeo:**
Msalaba Mwekundu wa Ufini: Fanya hivi, ukikutana na ubaguzi wazi.

## 1



**Ubaki na utulivu.**

Hisia zinaweza kupanda, lakini utulivu utakusaidia kuchukua hatua kwa njia ya kueleweka na kuleta matokeo.

## 2



**Omba uungaji mkono na msaada kutoka watu waliopo.**

Kama hali ni ya kutisha, piga simu huduma za dharura namba 112. Kumbuka usalama wako mwenyewe.


## 3



**Komesha hali.**

Komesha hali kwa kusema kwa utulivu, kwamba kitendo kinapaswa kukomeshwa.

## 4



**Sahihisha dhana zenye ubaguzi.**

Kama unasikia kauli za ubaguzi, unaweza kusahihisha au kubisha dhana hizo kwa utulivu na ustaarabu.

## 5

**Kaa pembeni.**

Kama hutaki kuongea, unaweza kukaa na kuunga mkono kwa yule anayekabiliwa na ubughudhi wa ubaguzi.



## 6

**Onyesha huruma.**

Ongea baadaye na yule aliyekabiliwa na ubaguzi na umwonyeshe huruma.

## 7

**Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**

Usikubali kutusiwa. Kutusiwa inaweza kuwa kitendo cha adhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Jinai (kashifu). Unaweza kutoa taarifa ya uhalifu juu ya jambo hilo.

# Mitandao ya kijamii, Anga za Burudani na Michezo

Unaweza kutoa dokezo kwa Polisi mtandaoni.

Anwani ya mtandao:
Polisi: Dokezo kupitia mtandao.

**Rejeo:**
Maneno ya chuki kwenye mitandao ya kijamii. Usaidizi kwa wenye mamlaka kuhusiana na matukio ya maneno ya chuki kwenye mitandao ya kijamii.

## 1



**Usichochewe.**

Jaribu kuwasiliana kwa ustaarabu. Pia unaweza kukataa kujibu.


## 2



**Hifadhi ushahidi.**

Hifadhi papo hapo ujumbe, picha na nyenzo zingine, ambazo ni za kukubughudhi. Piga picha ya kiwamba cha nyenzo zilizomo, maelezo mafupi ya mwandikiaji na anwani yake ya www.


## 3




**Ripoti yule aliyeandika.**

Toa ripoti kwa wasimamizi wa tovuti, mchezo wa mtandao au huduma ya mtandao.

## 4




**Bloki, yaani umzuie yule aliyeandika.**


## 5

**Tafuta msaada.**

Ongea na mtu au mtaalam anaye-aminika.




## 6




**Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**

Suala la jinai linaweza kutolewa ripoti ya uhalifu kwa Polisi. Panapohitajika, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai zinaweza kusaidia kuendeleza suala.


Pia unaweza kutuma dokezo kwa Polisi kupitia mtandao. Dokezo kupitia mtandao siyo ripoti ya uhalifu.

# Ufanyaji wa Maamuzi ya Kisiasa na Mazungumzo ya Umma

Jifahamishe na kampeni ya Msalaba Mwekundu wa Ufini ya kupinga ubaguzi.

Anwani ya mtandao: Msalaba Mwekundu wa Ufini: Rasisminvastainen viikko.

## 1



**Ubaki na utulivu.**

Utulivu utakusaidia kuchukua hatua kwa njia ya kueleweka na kuleta matokeo.


## 2



**Tafuta msaada.**

Zungumzia hiyo hali pamoja na watu wanaoaminika na omba msaada wao. Huwa ushirikiano unaweza kuleta mafanikio zaidi.

3



**Sahihisha dhana zenye ubaguzi.**

Kama unasikia kauli za ubaguzi, unaweza kusahihisha au kubisha dhana hizo kwa utulivu na ustaarabu.

4



**Shiriki katika harakati za kupinga ubaguzi.**

Unaweza kujiunga na mashirika au makundi, ambayo yanafanya kazi za kupambana na ubaguzi na kuendeleza usawa wa watu wote.

5

**Toa mchango wako kwenye majadiliano ya umma.**

1. Media na idhaa za mazungumzo: Shiriki au pendekeza mada mbalimbali kwa idhaa za mazungumzo kwenye media.

2. Makala ya maoni: Andika makala ya maoni na tume ujumbe kwa watu wanaofanya maamuzi.

3. Matukio ya mazungumzo: Andaa tukio la mazungumzo kwa mfano kwenye jumuiya yako ya kazi au uombe liandaliwe na wahusika wenye uwezo.

4. Miswada ya wananchi: Unaweza kujaribu kubadili sheria kwa kutoa muswada wa wananchi.


6 **Toa malalamiko juu ya mwenye mamlaka.**

Unaweza kutoa malalamiko juu ya utendaji wa mwenye mamlaka wa kieneo kwa Idara ya Utawala wa Jimbo. Malalamiko juu ya mwakilishi wa Baraza la Mawaziri yanaweza kutolewa kwa Kansela wa Sheria.

7 **Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**

Suala la jinai linaweza kutolewa ripoti ya uhalifu kwa Polisi. Panapohitajika, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai zinaweza kusaidia kuendeleza suala.

# Vyuo vya Elimu



1



**Omba mtu aache.**

Mtu akikutendea visivyofaa, mwambie anakosea namna gani na umwombe aache.

2



**Hifadhi ushahidi.**

Hifadhi papo hapo ujumbe, picha na nyenzo zingine, ambazo ni za kukubughudhi. Weka kumbukumbu matukio, nyakati na wahusika.


3

**Toa taarifa kwa wafanyakazi.**

Ongea kwanza kwa mfano na mwalimu, mwelekezi, mfanyakazi wa kijamii wa shule, mwuguzi, mwalimu mkuu au mwasiliani wa matatizo ya bughudha. Pia chuo cha elimu kinaweza kuwa na njia ya kutoa ripoti bila jina. Kama uko na umri mdogo, eleza shida yako kwa mlezi wako au mtu mzima salama mwingine.

Eleza kwa usahihi iwezekanavyo tu yale yaliyotokea, lini na wapi.

4



**Fuatilia taratibu za kuchukua hatua za chuo cha elimu.**

Fuatilia kama chuo cha elimu kiko na maelekezo (taratibu), jinsi gani hali inaweza kuingiliwa kati.

5 **Tafuta msaada kwa kujadilia tukio.**

Ikihitajika, unaweza kuwasiliana na:

- Huduma za Usuluhishi
- Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai (RIKU)
- Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi
- Mchunguzi Maalum wa Usawa wa Kijinsia au
- Idara ya Utawala wa Jimbo (AVI)

Hali ikifuatiliwa, wenye wajibu na walioshiriki wanapaswa kuwepo.



6


**Fuatilia, kwamba suala linaendelea na litasuluhishwa.**

7

**Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**

Suala la jinai linaweza kutolewa ripoti ya uhalifu kwa Polisi. Panapohitajika, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai zinaweza kusaidia kuendeleza suala.

# Sehemu ya kazi



**Marejeo:**
[Idara ya Utawala wa Jimbo (2024).]
[Ulinzi wa Kazi (2024).]
[Shirika la Wataalam Pro (2024).]

1



**Omba mtu aache.**

Mtu akikutendea visivyofaa, mwambie anakosea namna gani na umwombe aache.


2



**Hifadhi ushahidi.**

Kama una ushahidi wa matukio, uuhifadhi. Kwa mfano barua pepe au ujumbe. Weka kumbukumbu matukio na nyakati.


## 3



**Toa taarifa kwa msimamizi.**

Kama tabia hazitabadilika, wasiliana na msimamizi. Msimamizi akifanya makosa, wasiliana na mkuu wake.

## 4



**Fuatilia taratibu za kuchukua hatua za sehemu ya kazi.**

Fuatilia kama kwenye sehemu ya kazi kuna mwongozo au taratibu za kuchukua hatua kwa kuingilia kati utendeaji usiofaa au ubughudhi.

## 5 Tafuta msaada kwa kujadilia tukio.

- Unaweza kuomba msaada kutoka kwa wakili wa wafanyakazi wa sehemu ya kazi, kutoka Ulinzi wa Kazi au Huduma za Afya za Kazi.
- Kama wewe ni mwanachama, omba ushauri kutoka shirika lako la wafanyakazi.
- Kwa mfano unaweza kuwasiliana na Mchunguzi Maalum wa Usawa wa Jinsia, Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi au Idara ya Utawala wa Jimbo (AVI).



## 6

**Fuatilia, kama suala lako linaendelea kushughulikiwa kwenye sehemu ya kazi.**

Panapohitajika utapata maelekezo zaidi kupitia huduma za simu za Mamlaka ya Ulinzi wa Kazi.

## 7

**Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**

Suala la jinai linaweza kutolewa ripoti ya uhalifu kwa Polisi. Panapohitajika, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai zinaweza kusaidia kuendeleza suala.

# Michezo ya Kuburudisha na Muda Huru



**Rejeo:**
[Msalaba Mwekundu wa Ufini: Fanya hivi, ukikutana na ubaguzi wazi.]

1




### Fanya tukio lionekane.

Mtu fulani akikutendea visivyofaa, umwambie anakosea nini, na umwombe aache. Omba msaada kutoka kwa watu wengine waliopo. Ubaki na utulivu na zingatia usalama. Kama hali ni ya kutisha, piga simu huduma za dharura namba 112.

2



### Hifadhi ushahidi.

Hifadhi papo hapo ujumbe, picha na nyenzo zingine, ambazo ni za kukubughudhi. Weka kumbukumbu matukio, nyakati na waliohusika.


## 3



**Eleza kwa msimamizi.**

Eleza kwa mfano kwa mwelekezi wa michezo ya kuburudisha, kwa kocha au msimamizi mwingi. Ikihitajika omba msaada kutoka kwa wazazi, marafiki au watu wazima wengine wanaoaminika pia.

## 4



**Tumia taratibu za shirika la michezo ya kuburudisha.**

Fuatilia, kama shirika au jumuiya ya michezo ya kuburudisha wana taratibu za kuchukua hatua endapo visa vya ubaguzi au ubughudhi vinatokea.

## 5

**Tafuta msaada.**

Zungumzia suala lako pamoja na watu wako wa karibu, marafiki wanaoaminika au huduma za usaidizi, kwa mfano pamoja na Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai (RIKU) au Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi.



## 6

`poliisi.fi/tee-rikosilmoitus`

**Ikihitajika, wasiliana na Polisi.**

Suala la jinai linaweza kutolewa ripoti ya uhalifu kwa Polisi. Panapohitajika, Huduma za Dharura za Wahanga wa Jinai zinaweza kusaidia kuendeleza suala.

# Watumishi wengine

**Rejeo:**
Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi: Je, nimebaguliwa? Watendaji wengine.

### Mchunguzi Maalum wa Usawa wa Jinsia

Ukiwa na mashaka, kwamba umebaguliwa kutokana na jinsia, utambulisho wa kijinsia, uonyeshaji wa jinsia, uzazi au jukumu la kutunza familia, mwenye mamlaka aliye na madaraka ya kuchukua hatua ni Mchunguzi Maalum wa Usawa wa Jinsia. Maelezo zaidi utapata kupitia tovuti ya Mchunguzi Maalum wa Usawa wa Jinsia.

### Idara ya Utawala wa Jimbo (AVI)

Idara ya Utawala wa Jimbo inashughulikia kwa mfano malalamiko yahusikayo na elimu na elimu ya awali, madai ya rufaa, matamko pamoja na maombi ya rufaa ya makadirio ya wanafunzi. Kwa mfano rufaa kuhusiana na maamuzi ya uchaguzi wa wanafunzi inapaswa kutumwa kwa Idara ya Utawala wa Jimbo.

Pia AVI inaongoza na kufuatilia huduma za jamii za manispaa na za binafsi, pamoja na huduma za afya za umma na za binafsi. Maelezo zaidi utapata kupitia tovuti ya Idara ya Utawala wa Jimbo.

### Baraza la Usawa wa Kijinsia na Kupinga Ubaguzi

Baraza la Usawa wa Kijinsia na Kupinga Ubaguzi ni mamlaka ya ulinzi wa kisheria inayojitegemea, ambayo inatoa ulinzi wa kisheria kwa watu, ambao wanahisi wamebaguliwa. Baraza la Usawa wa Kijinsia na Kupinga Ubaguzi inaweza kubaini kisheria, kama ukiukaji wa marufuku ya ubaguzi ya Sheria ya Usawa umefanyika kwenye kesi. Uendeshaji wa kesi barazani hauna malipo. Maelezo zaidi kuhusu baraza hilo utapata kupitia tovuti ya baraza.

**Mchunguzi Maalum wa Kuwawakilisha Wagonjwa**
Endapo hujaridhika na matibabu ambayo umepata au ukihisi umetendewa visivyofaa kwenye huduma za afya, unaweza kuwasiliana na Mchunguzi Maalum wa Kuwawakilisha Wagonjwa. Kazi ya Mchunguzi Maalum wa Kuwawakilisha Wagonjwa ni kutoa ushauri na maelezo kuhusu hadhi na haki za mgonjwa. Maelezo zaidi utapata kupitia tovuti ya Valvira.

**Mchunguzi Maalum wa Masuala ya Huduma za Jamii**
Endapo hujaridhika jinsi ulivyotendewa au kuhudumiwa kwenye huduma za jamii, unaweza kuwasiliana na Mchunguzi Maalum wa Masuala ya Huduma za Jamii. Maelezo zaidi utapata kupitia tovuti ya Valvira.

**Senta ya Mikopo na Maendeleo ya Makazi (ARA)**
Senta ya Mikopo na Maendeleo ya Makazi (ARA) inafuatilia mipaka inayohusika na matumizi, uchaguzi wa wakazi na upangaji wa kodi za nyumba za kupanga za ARA.

**Huduma za Ushauri wa Bima na Fedha**
Huduma za Ushauri wa Bima na Fedha (FINE) inatoa ushauri kwa wateja kwa mfano kuhusu matatizo yanayohusika na masuala ya bima na benki. Maelezo zaidi utapata kupitia tovuti ya FINE.

**Kuomba mwenyewe ufafanuzi kutoka mtumishi**
Katika matukio fulani, inaweza kuwa ya maana zaidi mtu mwenyewe akiomba majibu kwa maandishi kutoka mtumishi anayeshukiwa na ubaguzi, kwa nini mambo yamefanyika vile katika hali husika. Hilo pekee linaweza kuleta suluhu. Kama suala litatolewa malalamiko baadaye kwa mfano kwa Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi, jibu kama hilo linaweza kuharakisha ushughulikiaji wa kesi kwenye ofisi ya mchunguzi.



# Viungo vyenye faida

**Harakati za kupinga ubaguzi:**

Anwani ya mtandao:
Msalaba Mwekundu wa Ufini: Harakati za kupinga ubaguzi.

**Toa ripoti ya uhalifu kwa Polisi:**

Anwani ya mtandao:
Polisi: Kesi za jinai.

**Jinai ya ubaguzi ni nini?**

Anwani ya mtandao:
RIKUteema: Jinai za ubaguzi.

**Wasiliana na Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi:**

Anwani ya mtandao:
Mchunguzi Maalum wa Kupinga Ubaguzi: Huduma za wateja.

**Maelezo juu ya jinai za chuki:** Poliisi: Viharikokset.

**Elimu ya mtandao kuhusu upingaji wa ubaguzi kwa wataalam:**
Thl.fi: Verkkokoulutus antirasismista ammattilaisille.

**Mwanasheria anajibu: Kitendo cha ubaguzi kinachotendwa kwa mtu ambacho kinaweza kuhukumiwa kisheria nchini Ufini?**
Rikosuhripäivystys: Juristi vastaa.

**Mfano, ambao unaweza kutumia kwa ajili ya kuandaa mwongozo wa taratibu za kuchukua hatua kwa jumuiya yako ya muda huru au shirika la michezo ya kuburudisha:** Sivista: Malli menettelytapaohjeiksi syrjintä- ja häirintätapauksissa.

**Mwongozo kwa aliyekabiliwa na ubaguzi** ni zana ya usaidizi kwa wote, ambao wamewahi kukabiliwa au kushuhudia ubaguzi, walio watu wa kuunga mkono kwa yule aliyekabiliwa na ubaguzi au wanaotaka kupata taarifa za awali, inafaa kufanya namna gani ukikabili vitendo vya ubughudhi wenye ubaguzi. Mwongozo huu unawasihi watu wote kupambana pamoja dhidi ya ubaguzi na kwa njia salama. Taratibu mbalimbali za kueleweka za kuchukua hatua zipo kwa kusaidia katika matukio tofauti, ambapo unaweza kukabili ubaguzi. Unapata ushauri, kwa mfano msaada unaweza kutafutwa kutoka wapi, kama mtu fulani anaonyesha tabia za ubaguzi kwa mfano kwenye sehemu ya kazi, michezo ya kuburudisha au katika majadiliano ya umma.

**Mwongozo umefanyika kwa kushirikiana na Rovalan Setlementti ry, Kitengo cha Jimbo la Lappi cha Msalaba Mwekundu wa Ufini na Mister's ry pamoja na kushirikiana na wataalam wa kazi na taaluma mbalimbali. Kwa msaada wa mwongozo huu, mipango ya kieneo ya kuchukua hatua za kupambana na ubaguzi na kuendeleza ushirikiano mzuri wa watu katika jamii inatekelezwa. Uandaaji wa mwongo huu umedhaminiwa na mradi wa Hyvät väestösuhteet.**

ROVALA ROVALA-OPISTO ROVALA MONINET Monikulttuurinen työ

Elinkeino-, liikenne- ja ympäristökeskus

Punainen Risti Lapin piiri

Euroopan unionin rahoittama

HVS HANKE HYVIEN VÄESTÖSUHTEIDEN EDISTÄMISEKSI

Monikulttuurinen miesten kerho Multicultural Men's Club Mister's RY